KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 13, Issue 3

19th Ramadhân 1432

19th Aug, 2011

YALIYOMO

SWALA YA 'EID MBILI 1 - 3

SUNNAH ZA 'EID 3 - 4

"SWALA YA 'EID MBILI

Na: Sheikh Muhammad Bin 'Umar Bin Salim Baazmul

Mlango huu umekusanya vipengele vifuatavyo:

1. HUKMU YA SWALA YA 'EID MBILI

Swala ya 'Eid ni waajib kwa kila Muislamu mwenye kuweza kuitekeleza, mume au mke katika mahala anapoishi. Na dalili juu ya hilo ni hadeeth aliyoipokea Umm 'Atiyyah (رضي الله عنها) amesema: "Alituamrisha (Mtume (صلى الله عليه وسلم)) tuwatoe wende kwenye swala ya 'Eid mbili; wanawali waliojisitiri (mabikra) na wanawake waliofikia kuolewa, ambao hawajaolewa. Na amewaamrisha wenye heidh wajitenge na sehemu za wanaoswali Waislamu. [Bukhaari na Muslim]. Jueni yakuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alidumu kuziswali 'Eid mbili na wala hakuwacha kuswali 'Eid yoyote, na aliwaamrisha watu kutoka kwenda katika Ibaada hiyo hata akawaamrisha wanawake oia watoke kwenda katika Ibaada hiyo, na akawaamrisha wanawake wenye heidh wajizuiye kuswalilakini waishuhudie kheri hiyo na washuhudie da'wah ya Waislamu kwa umuhimu wake hata akaamrisha ambaye hana JILBAAB (vazi la ki-sheriya) avae la ndugu yake. Na jambo la kuamrishwa kutoka laonyesha umuhimu wa kwenda kuswali kwa ambae hana udhuru kwa ufahamu wa mazungumzo hayo. Wanaume kwa hilo la kuamrishwa kuswali ni bora zaidi (kwao—wanaume) kuliko wanawake. Na dalili hizi zajulisha juu ya (uwajibu) ulazima wa swala ya 'Eid, tena uwajibu uliotiliwa nguvu kwa watu wote, si kwa baadhi yao.

2. WAKATI WA SWALA YA 'EID MBILI

Mas'ala Ya Kwanza: Wakati Wa Swala Ya 'Eid Mbili:

Imepokewa kutoka kwa Yazeed Bin Khumayree ar-Rahbee yakwamba amesema: "Alitoka Abdillaah Bin Busr, swahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) pamoja na watu katika siku ya 'Eid al-Fitr au adh-ha, akachukia kuchelewa kwa Imaam. Akasema, 'Sisi (wakati wa Mtume (صلى الله عليه وسلم)) tulikuwa tumeshamaliza kuswali katika muda huu.' Na huo ulikuwa ni wakati wa swala ya Dhuhaa. [Amepokea hadeethy hii Abu Daawud na Ibn Maajah].

NENO LA BUSARA

TANABAHI EWE NDUGU YANGU KATIKA SUNNAH!!

TWAFUNGA SAUMU NA KUFUNGUA SAUMU?

AU

TWAFUNGA MUADHINI NA KUFUNGUA MUADHINI?

Na hadeeth hii hujulisha yakwamba wakati wa swala ya 'Eid huanza wakati wa kuchomoza Jua na hujulisha pia juu ya Sunnah ya kutoka mapema katika swala ya 'Eid. [Tizama Fat-hul Baaree Juzuu 2 Uk. 457]. Amma mwisho wa wakati wake, wengi wa wanavyuoni wameonelea ni baada ya kupinduka kwa Jua (saa sita mchana) [Angalia Fat-hul Baaree Juzuu 2, Uk. 457]. Na baadhi yao wamekataa hoja hiyo kutokana na hadeeth ya Abdillaah Bin Busr.

Mas'ala Ya Pili: Hakuna katika swala ya 'Eid Adhaan wala Iqaamah:

Hakuna dalili katika swala ya 'Eid kuadhini wala kuqimu, wala kusema 'Swalaatul Jaami'ah'. Na dalili juu ya hilo, imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas na Jaabir bin Abdillaah al-Answaree yakwamba wamesema hakuwa Mtume akiadhini katika 'Eid al-Fitr wala 'Eid al-Adh-ha. Kisha nikamuuliza baada ya muda kutokana na hilo akaniambia: "Amenipasha habari Jaabir bin Abdillaah al-Answaaree yakwamba hakuna adhaan katika swala ya siku ya 'Eid al-Fitr wakati anapokuja Imaam wala baada ya kutoka, wala hakuna Iqaamah wala mwito wa aina yoyote." [Bukhaari na Muslim]. Amepokea Jaabir bin Samrah yakwamba amesema: "Niliswali pamoja na (صلى الله عليه وسلم) swala ya 'Eid Mbili, si mara moja wala mara mbili, pasi na adhaan wala Iqaamah. [Muslim]

Mas'ala ya Tatu: Idadi Ya Rakaa'ah Za 'Eid Mbili Na Takbira Zake:

Swala ya 'Eid mbili ni rakaa'ah mbili, na ataleta takbira katika rakaa'ah ya kwanza takbira saba kabla ya kusoma. Na ataleta katika rakaa'ah ya Pili, takbira tano, isiyokuwa takbira ya kuhama kutoka sehemu moja hadi nyengine kabla ya kusoma. Na dalili juu ya hilo, imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas: "Hakika Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali siku ya 'Eid ul-Fitr rakaa'ah mbili. Hakuswali kabla yake wala baada yake. Kisha akawaendea wanawake baada ya hapo pamoja na Bilaal. Akawaamrisha kutoa swadaka, wakawa wanawake wanatoa mikufu yao na vipuli vyao." [Bukhaari na Muslim].

Imepokewa kutoka kwa 'Umar (رضي الله عنه) yakwamba amesema: "Swala ya Dhuhaa ni rakaa'ah mbili na swala ya 'Eid ul-Fitr ni rakaa'ah mbili na swala ya msafiri ni rakaa'ah mbili , na swala ya Ijumaa ni rakaa'ah mbili zilizokamilika wala hazina upungufu kwa ulimi wa Mtume wenu." [an-Nasaa'ee].

Amma takbeer, dalili juu ya hilo ni yaliyopokewa kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها): "Kwa hakika Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akileta takbira katika 'Eid ul-Fitr na 'Eid ul-Adh-ha,

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

katika rakaa'ah ya kwanza, takbira saba na katika rakaa'ah ya pili, takbira tano. [ukitoa takbira mbili za ruku'] [Abu Daawud]. Na imepokewa kutoka kwa Abillaah bin 'Amr bin al-'Aass yakwamba amesema: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Takbira katika 'Eid ul-Fitr, katika rakaa'ah ya kwanza ni saba na tano katika rakaa'ah ya pili. Na kisomo ni baada ya hizo takbira.'" [Abu Daawud].

Mas'ala Ya Nne: Kisomo Katika 'Eid Mbili:

Husomwa katika rakaa'ah mbili Surat al-Faatiha kutokana na maneno yake Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Hakuna swala kwa asiyesoma Surat al-Faatiha." [Bukhaari na Muslim]. Na husomwa katika rakaa'ah mbili baada ya kusoma surat al-Faatiha kisomo chenye wepesi. Na imependekezwa kusoma kwenye rakaa'ah hizo mbili, Surat [Qaaf Wal-Qur'aanil Majeed] na Surat [IQTARABAT AS-SAA'ATU WANSHAQAL QAMAR]. Na husomwa kwa sauti ya Juu. Au husomwa kwenye rakaa'ah hizo mbili, Surat [SABBI HISMA RABBIKAL A'LAA] na Surat [HAL ATAAKA HADEETHUL GHAASHIYAH].

Na dalili ya hayo, imepokewa kutoka kwa Abee Waaqid al-Laythee yakwamba amesema: "'Umar Ibn al-Khattaab aliniuliza kuhusu sura alizokuwa akisoma Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika siku ya 'Eid." Nami nikamjibu: "Kwa [IQTARABATUS SAA'A] na [QAAF WAL QUR'AANIL MAJEED] [Muslim].

Amepokea an-Nu'maan Bin Basheer: "Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisoma kwenye swala za 'Eid mbili na katika swala ya Ijumaa [SABBI HISMA RABBIKAL A'LAA] na Surat [HAL ATAAKA HADEETHUL GHAASHIYAH]." Akasema: "Na zinapoingiliana 'Eid na Jumu'ah kwenye siku moja, huzisoma tena ndani yake." [Muslim].

3. SWALA YA 'EID MBILI KATIKA MUSWALLA NI SUNNAH

Sunnah ni kwa Imaam au msaidizi wake kutoka kwa ajili ya kuswali swala za 'Eid Mbili na kuelekea kwenye Muswalla. Na wala haziswaliwi kwenye msikiti isipokuwa kwa udhuru fulani.

Na hilo haliwahusu watu wa Maskkah, Allaah Awazidishie utukufu na heshima. Kwani kwa hakika wao hawakuwahi kutueleza sisi yakwamba mmojawapo wa ma-Salaf aliwahi kuswali nao swala ya 'Eid isipokuwa kwenye msikiti wao." [Imaam ash-Shaafi'ee Juz 1; Uk. 234]. Na miongoni mwa dalili yakwamba swala za 'Eid huswaliwa kwenye muswalla ni kama zifuatazo:

1. Yaliyowahi kupokewa kwenye hadeeth ya Umm 'Atiyyah kutokana na amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ya kuwaambia watoke na kuelekea kwenye muswalla.
2. Yaliyopokewa kutoka kwa Ibn 'Umar: "Yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa akitoka katika siku ya 'Eid huamrisha aekewe mbele yake Mkuki (au Ngao) na anaswali kuuelekea Mkuki huo, haliyakuwa watu wako nyuma yake. Na alikuwa akilifanya hilo katika safari na pia wakalifanya hilo viongozi waliokuja baada yake. Na katika riwaya nyengine: "Hakika Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akikita Mkuki mbele yake siku ya 'Eid ul-Fitr na adh-ha. Na katika riwaya nyengine alikuwa akitoka mapema sana kuelekea katika Musalla na Mkuki ukiwa mbele yake, nae akiswali hali ya kuuelekea. [Bukhaari na Muslim].

4. KHUTBAH BAADA YA SWALA YA 'EID

Khutbah katika 'eid mbili huwa baada ya swala, dalili juu ya hilo ni kama ilivyokuja kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) yakwamba amesema: "Nilishuhudia 'Eid pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم), Abu Bakr, 'Umar na 'Uthmaan (رضي الله عنهم); wote walikuwa wakiswali kabla ya Khutbah." [Bukhaari na Muslim]. Na imepokewa kutoka kwa Ibn 'Umar yakwamba amesema: "Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Abu Bakr na 'Umar (رضي الله عنهم), walikuwa wakiswali 'Eid mbili kabla ya Khutbah.

5. ZITAKAPOKUSANYIKA 'EID NA JUMU'AH

Ikikusanyika 'Eid na Jumu'ah, mwenye kuswali 'Eid hatowajibika kuswali Ijumaa, na badala yake ataswali swala ya Adhuhuri. Dalili juu ya hilo ni kutoka kwa Abu Hurairah (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba amesema: "Imekusanyika katika siku yenu hii ya leo, 'Eid mbili, anaetaka itamtosha 'Eid na aiwache Ijumaa, lakini sisi tutaswali." [Abu Daawud na Ibn Maajah]. Na imepokewa kutoka kwa 'Ataa bin Abee Rabaah: "Alituswalisha sisi Ibn az-Zubayr siku ya 'Eid ambayo ilikuwa ni siku ya Ijumaa, kisha sisi tukaelekea kwenda kuswali Ijumaa, hakutoka (kuja kutuswalisha), kwahivyo tukaswali kila mmoja peke yake, na Ibn 'Abbaas wakati huo alikuwa Taif. Aliporudi, tukamuuliza suala hilo, akatujibu yakwamba, Ibn az-Zubayr amepatia Sunnah." [Abu Daawud].

6. **ATAKAEKOSA SWALA YA 'EID ATASWALI RAKAA'AH MBILI**

Ikimpita Muislamu swala ya 'Eid, itambidi aswali rakaa'ah mbili, mfano wa swala ya Imaam katika 'Eid. Na dalili ya hilo ni hadeeth zifuatazo: Imepokewa kutoka kwa 'Aisha (رضي الله عنها) yakwamba amesema: "Aliingia Abu Bakr (nyumbani kwangu) na nilikuwa na vijakazi wawili wa ki-Answaar wakiimba wimbo ma-Answaar katika siku ya Bi'aath. Abu Bakr akawaambia: 'Munaleta mizumari ya Shetwani katika nyumba ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)?'. Na hilo lilikuwa katika siku ya 'Eid. Baada ya kuyasikiya hayo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: 'Ewe Abu Bakr, hakika kila watu huwa na 'Eid zao, na hii ni 'Eid yetu leo.'"

Na katika riwaya nyengine: 'Abu aliingia kwa 'Aaisha akamkuta nao wajakazi wawili katika siku za Minaa wanapiga Dufu na Mtume amejifunika nguo zake, Abu Bakr akawakemea. Mara Mtume (صلى الله عليه وسلم) akafungua Uso wake na akasema: "Waache hao Ewe Abu Bakr, hakika hii ni siku ya 'Eid." Na siku hizo zilikuwa ni siku za Minaa. Njia za kuifanya kuwa hiyo ni dalili ni kwamba kwanza Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliita kuwa ni siku ya 'Eid, akaiegemeza siku hiyo na tamko la 'Eid. Kwahivyo, huwa sawa katika kuisimamisha ile 'Eid mtu peke yake au pamoja na jamaa'ah na wanawake na wanaume. Hutilia nguvu kauli hii ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika riwaya ya mwanzo aliposema : "Hii ni 'Eid yetu," kwa maana yakwamba ni 'Eid kwa Waislamu. Na Waislamu ni neno lililoenea kwa wote hao. Na huko kuitwa kwake yakwamba ni siku za "Eid", inamaanisha kwamba hapo ni mahala palipoandaliwa kwa kuswaliwa 'Eid. Tunapata faida yakwamba yule anaekuja katika swala haliyakuwa amechelewa, akiswali rakaa'ah mbili, basi kwake ni sawa, kwa sababu wakati wa mwisho wa kutekeleza hilo la swala linamalizikia mwishoni mwa Minaa kwa mnasaba wa 'Eid al-Adh-haa [Fat-hul Baaree Juz 2; Uk. 475].

Amepokea Ubaydillaah bin Abee Bakr bin Anas bin Maalik, mtumishi wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Alikuwa Anas akikosa swala ya 'Eid pamoja na Imaam, hukusanya watu wa nyumbani kwake akaswali nao mfano wa swala ya Imaam katika 'Eid." [Al-Baihaqee]. Na amepokea Ibn

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Jurayj kutoka kwa 'Ataa yakwamba amesema: "Ataswali rakaa'ah mbili na huku akipiga Takbira." [Abee Shaybah]. Imaam al-Bukhaari ameweka mlango katika swaheeh yake chini ya anwani, "Mlango: Pindi mtu atakapokosa kuswali 'Eid na jamaa'ah, ataswali rakaa'ah mbili." [Fat-hul Baaree Juz; 2, Uk. 474]. Na amesema Ibn al-Mundhir: "Atakaeikosa swala ya 'Eid, ataswali rakaa'ah mbili kama swala ya Imaam." [Angalia al-Iknaa'un Juz 1; Uk. 110]

7. **IKIWA HAIKUJULIKANA KUWA IMEINGIA 'EID MPAKA BAADA YA KUPINDUKA KWA JUA.**

Ikiwa haikujulikanwa kuingia kwa 'Eid ila baada ya kupinduka kwa jua, watatoka kuswali 'Eid siku ifuatayo. Na dalili iliyokuja katika hilo, imepokewa na Abee 'Umayree bin Anas kutoka kwa '*Amooma* wake kutoka miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba walikuja watu wakiwa kwenye vipando mpaka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakashuhudilia yakwamba wao waliuona mwezi muandamo jana, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaamrisha kufungua saumu zao na kesho yake wende kuswali 'Eid kwenye Musallah. [Abu Daawud, an-Nasaa'ee na Ibn Maajah].

8. **HAKUNA SWALA YA 'EID UKIWA SAFARINI**

Haikuwepo Sheriya ya kuiswali swala ya 'Eid katika safari, kwani haikunukuliwa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba aliswali au aliamrisha kuswaliwa swala ya 'Eid pamoja na wingi wa safari zake na kupeleka kwake majeshi ya Waislamu makubwa na madogo kwenye sehemu mbalimbali. Na haya ndiyo madhehebu ya Abee Haneefah, Maalik na Ahmad katika riwaya zilizokuwa wazi kutoka kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Amesema ash-Shaafi'ee na Ahmad katika riwaya ya pili: "Imeshurutishwa Kuqimiwa katika Ijumaa na wala sio katika 'Eid. Na wakasema madh-heb ya *Dhwaahiriyya* yakwamba si sharti kuqimu katika swala ya Ijumaa wala swala ya 'Eid. Amesema Ibn Taymiyyah (رحمه الله): "Na ambalo ni la sawa bila ya shaka ni kauli ya mwanzo."

Mimi nasema: "Na akiwa msafiri yuko katika mji ambao sio mji wake, basi inamlazimu yeye aswali pamoja na hao (wakaazi), kwani Waislamu wote, waume kwa wake walikuwa wakishuhudia 'Eid pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) pasi na kufarikiana, *Wallaahu a'lam*."

BAADHI YA SUNNAH ZINAZOHUSIANA NA 'EID MBILI

Na: Sheikh Muhammad al-Jibaaly

GHUSL: Riwaya kumuhusu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akitekeleza Ghusl kwa swala za 'Idd ni dha'eef. Hatahivyo, imepokewa yakwamba Waislamu wa awali walifanya hayo; kwa mfano:

A. **Ibn 'Umar (رضي الله عنه)**

Alikuwa akitekeleza ghusl siku ya Fitr kabla hajenda katika musalla.

B. **'Ali (رضي الله عنه)**

Mtu mmoja alimuuliza kuhusu ghusl, akamwambia, "Waweza kutekeleza ghusl kila siku ukitaka." Akasema, "Si hivyo, lakini (siku ambazo mtu atahitajika) kutekeleza ghusl." Akasema **(رضي الله عنه)**, "Siku ya Ijumaa, siku ya 'Arafah, siku ya Nahr, na siku ya Fitr."

C. **Sa'eed Bin al-Musayyib** (رضي الله عنه) **amesema:**

"Kuna Sunnah tatu za Fitr: Kutembea kuelekea kwenye musalla, kula kabla hujenda, na kutekeleza ghusl.

KUJIKWATUA KWA AJILI YA 'IDD

Amepokea Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) "Umar alileta kilemba cha hariri kutoka sokoni, akampelekea Mjumbe wa Allaah, na akamwambia, 'Ewe Mjumbe wa Allaah, chukuwa hiki na ujipambe nafsi yako katika siku ya 'Idd na siku utakapofanyiwa ziyara na wajumbe tafauti.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Nguo hii ni ya wale wasiokuwa na fungu (katika siku ya Qiyaamah)."* Kisha baada ya muda mrefu kupita, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akampelekea 'Umar kilemba cha hariri. 'Umar akaja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kilemba akamwambia, "Ewe Mjumbe wa Allaah! Wewe ulisema yakwamba nguo hii ni ya wale wasiokuwa na fungu (katika siku ya Qiyaamah), na kisha ukaniletea mimi!" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Kiuze na utekeleze mahitaji yako kwa hicho."*

Hadeeth hii ni dalili yakwamba Maswahaba walikuwa wakivalia vizuri katika Siku Kuu zao, na Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwakataza kufanya hivyo. Kwa hakika Ibn Hajar amesema: "Ibn Abu ad-Dun'yaa na al-Baihaqee wamepokea, kwa isnadi iliyo swaheeh ya wapokezi kutoka kwa Ibn 'Umar, yakwamba alikuwa akivaa nguo zake nzuri katika siku za 'Idd mbili ..."

Akanukuu Ibn Qudaamah, "Na hili lathibitisha yakwamba walikuwa wakiruhusiwa kujikwatua kwenye masiku haya. Amesema Maalik, 'Niliwasikiya wanavyuoni wakieleza kuhusu kupenda kujipaka manukato na kujipamba katika kila 'Idd.'"

Ibn al-Qayyim nae akasema: " Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akuvalia nguo zake nzuri akenda kuswali. Alikuwa na nguo makhsusi akizivaa kwa 'Idd mbili na siku ya Ijumaa. Siku moja alivaa kilemba cha rangi ya kijani na mara nyengine akavaa cha rangi ya nyekundu—lakini si cha rangi nyekundu mbichi kama watakavyodhani watu wengine, lakini kilikuwa na maridadi za rangi nyekundu kama kilemba cha ki-Yemen."

Al-Maqtari akanukuu: "Miongoni mwa mapambo ni kujitia wanja, mafuta mazuri na kuvaa *'amaamah* au kuvaa kofia. Na Waislamu wanaume wasiwache vichwa vyao wazi, kwa vile kuwa hivyo ni katika mila za Wazungu wa Ulaya kama ilivyotajwa na Sheikh al-Albaani katika *Tamaam al-Minnah*."

KULA AU KABLA YA KUONDOKA

Kutoka kwa Anas Bin Maalik (رضي الله عنه): "Mtume ((صلى الله عليه وسلم alikuwa hatoki kwenye siku ya Fitr mpaka kwanza ale tende."

Kutoka kwa Buraydah Bin al-Haseeb (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa hatoki kwenye siku ya Fitr mpaka kwanza ale. Katika siku ya Nahr (siku ya kuchinja) alikuwa haanzi kula mpaka akirudi ndipo anapokula mnyama aliyechinjwa."

KURUDI KUTOKA KATIKA MUSALLA KWA NJIA TAFAUTI

Kutoka kwa Jaabir Bin 'Abdillaah (رضي الله عنه)**:** "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akichukuwa njian tafauti katika siku za 'Idd."

Ibn al-Qayyim amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akichukuwa njia tafauti katika siku za 'Idd. Alikwenda kwa njia

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

moja na kurudi kwa njia nyengine. Wamesema yakwamba sababu ya hii ni kuwaamkuwa watu kwenye njia zote hizo mbili. Wengine wamesema yakwamba ni kupata baraka zilizopo za njia zote mbili. Baadhi nyengine wamesema ni kwa kuubainisha (kwa takbeer n.k) Uislamu, na wengine wamesema - na msemo huu wao ndio bora zaidi - ni kwa sababu zote hizi zilizotajwa na nyengine ambazo yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) azijuazo."

MWENDO WA KUTEMBEA

'Ali (رضي الله عنه) amepokewa kuwa amesema: "Miongoni mwa Sunnah ni kwenda kwenye 'Idd kwa kutembea."

KULETA TAKBEER KATIKA 'IDD MBILI

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Na (anakutakieni) kumtukuza Allaah kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru."** [al-Baqarah 2:185]

Imethubutu yakwamba pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Alipokuwa akenda katika siku ya Fitr, alikuwa akileta Takbeer mpaka afike kwenye musalla, na mapaka amalize kuswali. Amalizapo kuswali, hunyamaza kuleta takbeer."

Mwanachuoni wa Hadeeth, Sheikh al-Albaani amesema: "Katika hadeeth hii ni dalili ya kuruhusiwa kwa yaliyo kawaida miongoni mwa Waislamu wengi ya kuleta takbeer kwa sauti wanapoelekea kwenye musalla ... Kulingana na sisi, kuleta takbeer kwa pamoja (sauti moja) kama wanavyofanya watu wengi ni jambo ambalo halikuamrishwa. Kila sampuli ya Dhikr imeamrishwa iwapo itamkwe kwa sauti au kuletwa kimya, lakini hakuna ruhusa ya kuleta Dhikr kwa sauti moja. Kwahivyo, hili ni **ONYO** kali dhidi ya kitendo hicho..."

Ama kuhusu wakati maalum ambao takbeer huanzishwa, ni wakati wote bila ya kuwa makhsusi. Maadamu hilo ndilo lililosemwa na Imaam al-Bukhaari katika *Kitaab ul -'Eidayn* cha Swaheeh yake:

Hukmu yake ni waajib kulingana na wengi, kwani yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwaamrisha peke yake watu wake wote kwa ujumla; "... Kwahivyo aliwaamrisha wao wafungue saumu zao, na watoke kwenda kwenye musalla ..."Hata Mtume (صلى الله عليه وسلم) pia aliwaamrisha makhsusi wanawake wote wakahudhurie; akasema Umm 'Atiyyah; Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) alituamrisha yakwamba wanawake wakuu na wanawali watoke na kuelekea, isipokuwa tu wanawake walio kwenye heidh wajitenge na musalla;

Na katika riwaya nyengine; "(Aliamrisha) yakwamba wanawake wakuu na wanawali na watoke kuelekea, isipokuwa walio kwenye heidh (miongoni mwao) na wajitenge na musalla." Amesema Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah ((رحمه الله: "Kwahiyo, sisi twajitegemeza kwenye maneno yakwamba *Swalaatul 'Idd* ni waajib kwa kila mtu (*al-'ayn*) kama alivyosema Abu Haneefah na wengineo. Huu ni mmojawapo wa misemo iliyopokewa kutoka kwa ash-Shaafi'ee na mmojawapo wa misemo miwili katika *madh-hab* ya Ahmad. Na inavyosemekana yakwamba si waajib inaonekana kuwa mbali na na ukweli, kwa sababu ni miongoni mwa alama kubwa za Uislamu, na watu wengi hujitokeza kuhudhuria kuliko swala ya Ijumaa. Na *takbeer* imehukumiwa itekelezwe (kuihusu aya). Na kusemekana yakwamba ni faradh kifaayah hakuna msingi ..." Akasema Ash-Shawkaani: "Jua yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliitekeleza swala hii katika kila siku ya 'Idd na wala hakuwahi kuiwacha, na akawaamrisha watu wajitokeze kwa wingi wakaihudhurie, hata aliwaamrisha wanawake wakuu, wanawali, na wanawake walio kwenye ada zao za kila mwezi wakahudhurie, akawaambia walio kwenye heidh wasiwe ni wenye kuswali, lakini wahudhurie tu kwenye 'amali hii nzuri kwa maombi pamoja na Waislamu wenzao. Hata Mtume (صلى الله عليه وسلم) pia akamuamrisha mwanamke ambae aliyekosa *Jilbaab* akaazime kutoka kwa rafikiye. Na yote hayo yanathibitisha yakwamba swala hii ni waajib juu ya kila mtu na wala sio *kifaayah,* na amri ya kutoka na kuelekea kwenye musalla imebaki licha ya kufutwa kwa amri ya kuswali kwa mwenye udhuru wa kutoswali...". Kisha akasema, "Na miongoni mwa dalili yakwamba ni waajib ni kwamba inaifuta hukmu ya swala ya Ijumaa zinapopambana (siku) zote mbili katika siku moja. Na lisilokuwa ni waajib haliwezi kufuta lile ambalo ni..." Katika kuisherehesha hadeeth ya Umm 'Atiyyah, Sheikh al-Albaani (رحمه الله) amesema: "Amri iliyotajwa hapa ni ushuhuda yakwamba ni waajib, na inapokuwa ni waajib kutoka na kwenda kwa ajili yake, basi inakuwa ni waajib kuiswali kwa mwenye kupaswa kuswali ...

KUTAMKA *TAKBEER* MWANZONI MWA KHUTBAH

Amma kuhusu kufungua khutbah kwa takbeer, hakuna riwaya iliyoswihi kutoka katika Sunnah kuhusu jambo hilo, na huu pia ndio msimamo wa Ibn al-Qayyim.'

KIKAO BAINA YA KHUTBAH MBILI

Hakuna hadeeth iliyo swaheeh ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) inayobainisha yakwamba khutbah ya 'Idd igawanywe sehemu mbili baina ya kikao kati yake.

MAAMKUZI YA 'IDD

Jubayr Bin Nafeer amesema, "Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikuwa wakikutana katika siku ya 'Idd baadhi yao walikuwa wakiwaambizana, *Taqabbala-Llwahu Minnaa Waminkum.* (Twamuomba Allaah atutaqabalie sisi na nyinyi). Amesema Muhammad Bin Ziyaad, "Nilikuwa pamoja na Abu Umaamah al-Baahilee na baadhi ya Maswahaba wengine wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Walipokuwa wakirudi kutoka kwenye swala ya 'Idd, baadhi yao walikuwa wakiambizana *Taqabbala-Llwahu Minnaa Waminkum.* (Twamuomba Allaah atutaqabalie sisi na nyinyi).

Kiwango cha maamkuzi ni kama hicho kilichotajwa kuhusiana na 'Idd. Haifai kwa wale wenye kupenda kufuata Sunnah kushikilia mila nyengine za watu wa sehemu zao katika maamkuzi ya 'Idd ambayo huwa na nyongeza juu ya mila hii ya Uislamu.